

Kila mmoja anayo Nafasi

Wakati mmoja kulimea kabichi moja kubwa shambani. Mkulima hakusubiri kuling'oa kabichi. Lilikuwa kubwa kwa hivyo angeliuza kwa pesa nyingi.

Lilipokuwa tayari mkulima aliamua kuling'oa. Alivuta, akavuta na kuvuta lakini hakufanikiwa! "Nitamwita mke wangu," mkulima alisema, alipogundua anahitaji msaada.

Mkulima na mkewe walivuta kabichi hilo kubwa, lakini hawakuweza kuling'oa. "Nitakwenda kumwita kijana wangu," mkewe alisema, kwa sababu walitambua wanahitaji msaada lakini hawakuweza kuling'oa kabichi. Walimwita dadake, mbwa na paka ili wawasaidie. Licha ya kutumia nguvu zao zote walishindwa kung'oa kabichi hilo kubwa.

Mwishowe ilibidi wamwite mnyama wa mwisho aliyekuwepo, panya mdogo, msaada. Hata hivyo ni mdogo sana na hawakuona kama anaweza kuchangia pakubwa.

Lakini panya alipojiunga nao, kabichi lilianza kung'oka. Wote kwapamoja wakawa na nguvu za kutosha kung'oa kabichi kutoka mchangani.

Watu wengi husema kuwa hadithi hii inahusu umoja katika utanda kazi jambo ambalo ni kweli. Vil vile inazungumzia nguvu, juhudi na mchango wa wale walio wanyonge, dhaifu na wasio na umuhimu wowote. Hii ni taswira na picha nzuri ambayo kuwa utaratibu wa juhudi katika kanisa na jamii kwa jumla. Tafakari maneno haya kutoka kwa 1 Wakorintho 12:21-24: "Na jicho haliwezi kuuambia mkono, 'Sina haja na wewe'; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, 'Sina haja na ninyi'. Bali zaidi sana vile viungo vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana. Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa."

Kila mmoja ni wa maana, anafaa na tuko sawa katika jamii ya Yesu.

Zingatia!

Ikiwa mna viongozi au wasio viongozi, 'wanaofaa' na 'wasiofaa' katika Vikundi vyenu vya Maisha au jamii, amua kuwachukulia watu wote kwa usawa.

Watambue watu wanaodharauliwa na kupuuzwa. Watie moyo, wape zawadi, washukuru hadharani kwa kuhusika na kuchangia kwao.


Omba:

- 1) Mungu atakuonyesha jinsi ulivyo wa maana katika jamii yenu.
- 2) Viongozi wa jamii yenu watawahimiza kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano.



"Kuna uwezekano kile tunachofanya si cha maana au labda ni upuuzi kwa wengine, lakini ninamaanisha ni umuhimu mno. Kinajenga jamii zetu kinaleta mabadiliko katika jamii zetu, kwa urahisi na wepesi uliopo."

- Gervas, Central Province, Zambia



Somo hili limedhaminiwa na: "Kila Mmoja Anakaribishwa" somo linalopatikana kwa kitabu cha Panda: Mafunzo ya Msingi ya Vikundi vya Maisha. Kinapatikana hapa:

dignityonline.org.uk/publications